MMEM ni Nini?

MMEM ni Nini?

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) ni programu ya Serikali ya kuboresha elimu ya msingi kwa watoto wote nchini. Hii inajumuisha wasichana na wavulana, matajiri na maskini, pamoja na watoto wenye ulemavu – hakuna hata mmoja atakayeachwa. Kwa kuwa hii ni programu ya kitaifa shule zote za msingi nchini zitafaidika. Huu ni mpango wa miaka mitano kuanzia 2002 hadi 2006.

Vipengele vikuu vya MMEM ni vipi?

MMEM ni mpango wenye mwelekeo mpana kwa maendeleo ya elimu ya msingi. Vipengele vyake vinne muhimu ni, ongezeko la uandikishaji, kuinua kiwango cha ubora, kujenga uwezo, na matumizi ya fedha na miundo ya kitaasisi. Mpango huu pia unalenga katika masuala muhimu ya jinsia na UKIMWI.

MMEM inatambua kwamba vipengele vyote vina umuhimu sawa, na kwamba vinategemeana. Kwa mfano haitoshi tu kuandikisha maelfu ya watoto shuleni kama walimu hawapo au kama kiwango cha elimu hakina thamani. Hii inaweza kusababisha watoto kuacha shule.

MMEM itaboreshaje upatikanaji wa elimu?

Kufuatana na MMEM, watoto wote waliko katika umri wa kwenda shule wataandikishwa katika shule za msingi ifikapo mwaka 2004. Ili kuhakikisha kwamba hakuna mtoto anayenyimwa fursa ya kwenda shule, Serikali imeifanya elimu ya msingi kuwa ya bure kwa kuondoa ada ya shule na michango yote ya lazima. Ili kukidhi ongezeko la uandikishaji, kati ya mwaka 2002 na 2006, vyumba vipya vya madarasa 54,000 (pamoja na vyoo) vitajengwa na walimu 46,000 zaidi wataajiriwa.



Kila shule inayohitaji vyumba vya madarasa vya ziada itapewa msaada wa fedha za maendeleo kwa ajili ya gharama za ujenzi. Wilaya zenye upungufu mkubwa zaidi, kama Kahama, zitapata msaada zaidi kuliko zile ambazo zinaupungufu kiasi. Jumuiya hazilazimiki kulipia gharama za ujenzi, lakini wanajamii watahamasishwa kuchangia muda na nguvu zao.


Kwa watoto wakubwa ambao hawajaandikishwa hadi umri wa miaka 10 au wale walioacha shule kwa sababu mbalimbali, Serikali itawapatia elimu isiyo rasmi kupitia mipango kama Mpango wa Elimu ya Msingi Kwa Walioikosa (MEMKWA). Nia ni kwamba watoto wote hapa Tanzania wapate kufurahia haki yao ya elimu ya msingi.

MMEM itainuaje kiwango cha ubora?

MMEM ina mpango wa kuongeza ubora wa elimu ya msingi kwa kuajiri walimu zaidi, na kwa kutoa mafunzo kazini kwa walimu na kwa wale ambao hawajaanza kazi, ambayo yanalenga katika mbinu za ufundishaji za kitaaluma, kirafiki kwa mtoto na zinazozingatia masuala ya kijinsia. Shule pia zitaweza kupata vitabu vya kiada vya kutosha.

MMEM itahakikishaje kuwepo kwa fedha za kutosha kwa ajili ya elimu?

MMEM inatambua kwamba ubora unahitaji fedha, na kwamba fedha zinahitaji kufika ngazi ya shule. Serikali imeahidi kwamba itatoa robo ya bajeti yake kwa ajili ya elimu, kati ya hizo asilimia 62 zitakwenda katika elimu ya msingi. Nchi za wahisani nazo zimeahidi kusaidia mpango wa Serikali kuziba mapengo yoyote katika bajeti yake. Cha muhimu zaidi, utaratibu wa ruzuku kwa kila mwanafunzi (capitation grant) umeanzishwa. Kwa hiyo Dola 10 za Marekani, takriban shilingi za Tanzania 10,000 kwa mwaka, kwa kila mtoto aliyeandikishwa, zitatumwa kwa kila shule kwa ajili ya kuboresha elimu.





MMEM itaboreshaje usimamizi wa elimu?

Kuwepo kwa vyumba vya madarasa, walimu, vitabu na fedha ni muhimu, lakini elimu lazima isimamiwe vizuri. Ndio maana basi, kuwa na miundo bora ya kitaasisi ni moja ya nguzo kuu nne za MMEM. Kufuatana na mabadiliko katika serikali za mitaa, shule zinatakiwa kusimamiwa kwa namna ambayo inazingatia ushiriki kamilifu wa watu.

Katika ngazi ya shule, kamati za shule zinazojumuisha wazazi na wanafunzi waliochaguliwa kidemokrasia zinatakiwa kuwa na nguvu na rasilimali ili ziweze kufanya maamuzi. Shule hazitawaliwi tena na "wakuu" wachache ila na wawakilishi wa watu kwa njia ya uwazi na ukweli. Maafisa wa wilaya hawatakiwi kutoa amri tu, badala yake waone majukumu yao ni kutoa huduma kwa jamii na wawajibike kwa matendo yao. Katika ngazi ya taifa, majukumu ya wizara husika yanahitaji kuainishwa, na uundaji wa sera utahusisha wadau wote, zikiwemo asasi za kiraia. Ili kuwezesha haya, mpango mkuu wa kujenga uwezo umepangwa, na umetiliwa mkazo katika ngazi za wilaya na jumuiya.

MMEM inasemaje kuhusu jinsia, UKIMWI na ulemavu?

Jinsia na UKIMWI vinatambulika kama masuala yanayogusa vipengele vyote vinne. Inatambulika kwamba wakati idadi ya wasichana na wavulana wanaoanza na kumaliza shule za msingi Tanzania ni karibu sawa, mazingira ya shule ni mabaya zaidi kwa wasichana. Mara nyingi wasichana hawapati nafasi sawa ya kushiriki darasani, mitaala inaendeleza mambo yanayomrudisha nyuma msichana, wasichana wanakosa mahitaji muhimu kama vyoo vinavyokidhi mahitaji yao na maji, na wana uwezekano mkubwa wa kunyanyaswa kijinsia. UKIMWI una athari kubwa kwa afya za walimu, na zaidi ya watoto milioni moja wamepoteza mzazi mmoja au wote wawili kutokana na ugonjwa huo. MMEM ina lengo la kushughulikia masuala haya moja kwa moja, lakini njia ambayo itatumika bado haijaainishwa. Mwanzoni mwa mwaka 2003 Waziri wa Elimu na Utamaduni pia aliagiza kwamba suala la ulemavu lijumuishwe katika MMEM.

Nitafahamuje zaidi kuhusu MMEM?

Kila mtu ana haki ya kupata habari, na kila mmoja ana haki ya kufahamu kuhusu MMEM. Kwa kuwa sasa unafahamu vipengele vya MMEM, unaweza kuona kama mambo yaliyotajwa yanatokea katika jumuiya yako na kama sivyo uliza maswali. Kwa mfano, unaweza kutathmini kama vipengele vyote vinne vya MMEM vinatekelezwa, unaweza kuuliza kama fedha za MMEM zinafika shuleni kwako, na kama zinatumika ipasavyo. Una haki ya kuuliza maswali na kupata majibu fasaha. Kwa mujibu wa mabadiliko ya Serikali, haikubaliki tena kwa kiongozi kutoa amri tu bila kuwasikiliza watu. Ni dhahiri mabadiliko huchukua muda, na hatutegemei kwamba kila kitu kitakuwa timilifu mara moja. Hata hivyo, una haki ya kuona maendeleo yakitokea katika maeneo yote muhimu ya MMEM.

Unaweza kupata habari kutoka kwa mwalimu mkuu, Afisa Elimu wa Wilaya, Diwani au Mbunge wako. Unaweza kuomba taarifa kutoka Mkutano wa Kijiji/Mtaa au vikao vya Halmashauri. Unaweza pia kuuliza Asasi Zisizo za Serikali (AZISE) katika eneo lako.



hakielimu

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania • Simu (022) 2151852 / 3 • Faksi (022) 2152449 • info@ hakielimu.org • www.hakielimu.org